

Title: Under the Mango Trees

EPISODE 1

Author: Romie Singh

Editors: Susanne Fuchs, Katrin Ogunsade, Maja Braun

Translator: Zainab Aziz Salim

List of characters for episode 1:

- Narrator
- Grandma
- April
- Desirée
- Endurance
- Lorraine
- Teacher
- Children in background
- Students in background

INTRO

Karibu kwenye mchezo wa redio wa Noa Bongo Jenga maisha Yako. Katika mfululizo wa sehemu kumi za mchezo mpya kwa jina “Chini ya Miembe” utajifunza mengi kuhusu mpango wa uzazi. Mchezo huu mura kabisa utawaeleimisha vijana jinsi ya kujikinga na mimba zisizotakikana, maambukizi ya virusi vya HIV na magonjwa ya zinaa kwa kuzingatia njia mbali mbali za mpango wa uzazi zilizopo. Katika sehemu ya kwanza tunapata kumfahamu msichana Desirée. Mama yake aliyetitwa April, alifariki wakati wa kujifungua. Desirée sasa anahangaika peke yake na mzigo wa kuwalea watano wadogo. Wakati huo huo anakabiliwa na wakati mgumu kwani nyanya yake ana mtazamo wa kizamani kabisa

kuhusu nafasi ya mwanamke katika familia . Hebu tega sikio ili upate kujua ni kipi kinacho mkasirisha msichana huyu mwenye umri wa miaka 16 au kipi kinachomfurahisha? Karibu kwenye sehemu ya kwanza ya mchezo kwa jina Chini ya Miembe.

***SIG.TUNE The song April sings is the one Desirée sings and should be the signature tune. HOLD UNDER 5-8 secs. AND FADE**

NARRATOR: Ni saa tisa alfajiri. Shambani kimya kimetanda. Miti ya miembe iliyo katika eneo la nyumba ndogo ya shamba pia imetulia tulii wala haitingishiki. Watu wa kijiji cha Mtelera wamelala fo fo fo. Lakini bibi mmoja anageuka geuka kitandani huku akiwa kwenye ndoto.

Sc.1 Night ambience. Inside the house. April singing*.

1. GRANMA: (gently) Mwanangu April – hebu jifunike khanga hii unapo mnyonyesha mtoto wako.
2. APRIL: (stops singing) Asante mama. (screaming) Ohh – Ohh. Haaah.
3. GRANMA: (panicking in sleep) April, hapana, hapana! Mungu wangu nisaidie. April, mwanangu.
4. DESIRÉE: (breathless) Nyanya Linda! Amka! amka!
5. GRANMA: (waking up) Uh? Nini?

6. DESIRÉE: Ulikuwa umekumbwa na jinamizi.
7. GRANMA: (in panic) April! Yuko wapi? (sobbing) Oh, mwanangu!
8. DESIRÉE: (gently) Shhh. Lala. Mama amepumzika sasa . Jaribu kulala nyanya.
9. SFX: Sobbing dies down.

Sc.2 In the bedroom.

10. SFX Crickets chirping outside. Door opens, closes. Endurance is crying softly.
11. ENDURANCE: (**Frightened**) Des? Kwa nini nyanya alikuwa napiga kelele? Kulitokea nini?
12. DESIRÉE: (**Sigh**) Alikuwa anamuota mama yetu –alikumbwa na jinamizi. Haya na wewe lala sasa.
13. ENDURANCE: Kwani Mama ni Mzimu?
14. DESIRÉE: Hapana, Endurance, yeye ni mzuka na hana raha namna alivyoatuacha.
15. ENDURANCE: (sniffing) Hata mimi, na baba? kwa nini nae alituacha?

16. DESIRÉE: Baba atarudi kuja kutuchukua hivi karibuni.
17. ENDURANCE: (calmer) Kwa nini Mama anamfanya nyanya apige kelele?
18. DESIRÉE: Nyanya ana majonzi. Wakati sisi mama yetu alipofariki na yeye ujue Aliondokewa na mwanawe. Mama yetu alikuwa mtoto wake.
19. ENDURANCE: (sniffing) Kwa nini Mama alikufa ? kwani tulimpigia kelele nyingi ? au sisi pia ndio tumemfukuza baba yetu?
20. DESIRÉE: Shh, Endurance – mimi sijui ni kwa nini alikufa lakini nafahamu hakufa kwa sababu eti sisi tulifanya kitu chochote na pia unajua ni kwa nini baba aliondoka kwa sababu alituambia kuwa ameenda kutafuta kazi. Shamba halikuwa likimletea fedha za kutosha.
21. ENDURANCE: (sleepy) Yuko Granville. Alihidi kuwa atakuja kutuchukua hivi karibuni.
22. DESIRÉE: (humming softly the song her mother sang) Shhh. Wacha tulale sasa. Tunahitajika kuamka mapema kesho. Usiku mwema!

23. SFX: MUSIC UP dream-like atmosphere.

NARRATOR: Endurance alizama kwenye usingizi mzito, na Desirée akatumbukia kwenye ndoto ambayo inamjia kila mara siku hizi – chini ya miembe, akizungumza na mama yake.

Sc.3 Outside in the mango grove

SFX: Wind in the trees.

24. DESIRÉE: (softly) Ei! Mbona kuna miti mingi hivi?

25. APRIL: (with echo) Kila mti mmoja unadhihirisha mauti katika familia yetu – kila mmoja unazaa matunda. Isipokuwa mimi siwezi kuzaa tena matunda – sitopata tena watoto zaidi.

26. DESIRÉE: Lakini mama una sisi watoto wako!

27. APRIL: (with echo) Ai, watoto wangu wazuri! Mwanangu pendwa Bella tayari yeye ni mwanamke! Na wewe mrembo wangu Des, baki hivyo hivyo ujilinde kwa muda mrefu kadri utakavyoweza. Tafadhali msaidie sana mwanangu wa kiume, Endurance, awe muungwana atakae waheshimu wanawake wote! (echo) Maisha yako ni yako.

28. DESIRÉE: Nitajitahidil Mama. - Mama? Ninataka kuwa mwimbaji. Unadhani nitaweza? Mama?
(Sadly) Oh! ameshaondoka.

29. SFX: MUSIC UP and OUT.

30. SFX Cock crows. Cooking noises, boiling kettle, sizzling. Fade under.

NARRATOR (brighter voice): Desirée ana miaka 16 tu lakini kila siku analazimika kuwaogsha na kuwavisha wapwa zake wanne . Hawa ni watoto wa mjomba wake Blessing. Aliwaacha kwa nyanya Linda baada ya kufiwa na mkewe. Watoto hawa walikuwa na majonzi makubwa tangu mama yao alipoaga dunia.

31. SFX: Children playing around (fade in)

Taratibu watoto hawa wadogo walianza kuwa na furaha , lakini Endurance alikasirishwa na kelele zao.

Sc.4 Early morning.. In the kitchen.

32. SFX: Distant cock crows. Wood stove. Children playing around in the background, coming to table.

33. DESIRÉE: Osha mikono yako kabla hujakaa kula chakula, Endurance.

34. ENDURANCE: (upset) Mikono yangu ni safi. Hebu nipe maziwa.

35. DESIRÉE: Endurance, hebu ngoja. Sio lazima uwe wa kwanza kwa kila kitu.
36. ENDURANCE: Nimechungu ng'ombe kama kawaida yangu kila asubuhi. Wewe umekamua ng'ombe wawili tu.
37. DESIRÉE: Watatu!
38. ENDURANCE: Na chai? Des? Hebu nitilie.
39. DESIRÉE: Tosha Endurance! Ndio wewe ni mwanaume hapa, lakini wewe ni mdogo kwa hiyo lazima uonyeshe heshima.
40. ENDURANCE: Baba alisema wanaume wanahudumiwa kwanza.
41. DESIRÉE: Hapana, hakusema hivyo, hata hivyo mimi ndio mwanaume sasa!
42. ENDURANCE: Unatamani! Wewe huvai suruali ndefu mimi navaa!
43. DESIRÉE: Mimi ni mwanaume na mwanamke pia. Ninawatunza nyote. Lakini nakiri kuwa wewe una miaka kumi na tatu sasa hivyo unafaa kujifanyia vitu vingine mwenyewe wewe ni

mkubwa sasa. Cahai iko jikoni na mkate uko kwenye kioka haya endelea kujihudumia kwani mimi ninataka kuwaogesa na kuwavalisha watoto.

44. ENDURANCE: (protesting) Lakini sihitajiki kujitengenezea kiamsha kinywa mimi mwenyewe!

45. DESIRÉE: (off mic) Na basi ujue tuna dakika 15 tu kabla basi letu halijaja.

46. NARRATOR: Shuleni, Desirée alicheza na rafiki yake mpendwa, Lorraine. – wote wawili walipenda kuimba!

47. SFX: Suggested lyrics for improvisation: Play with it. Have fun!

*We are the children, the new generation, the next of kin. We talk we sing
We carry the words forward that our elders taught us, we take from you
but we add our own.*

*We talk our talk and walk our walk and though we don't want to break the
chain*

*We do want to add our names and make our mark to make our own hall
of fame.*

Refrain: Value your children, the line of descent to the line of ascent.

Past and present. Etc.

Sc.5 In school yard. Background sound of kids shouting/playing

48. LORRAINE/DES: (Improvisation) Practising the song together.

49. TEACHER: (off mic) Desirée Thomas?

50. DESIRÉE: (on mic) Ssh, Lorraine! Mwalimu David anakuja (off mic) Naam mwalimu.

51. LORRAINE: Nini? Popo wa Jahanam?

52. DESIRÉE: (giggling) Shh-ana masikio makubwa akikusikia shauri yako!

53. TEACHER: (on mic) Mdogo wako Endurance leo alilala darasani. Na ananuka kama ng'ombe. Nitamfukuza shuleni iwapo atakuja namna hiyo tena. Pia nitawaandikia wazazi wenu barua.

54. DESIRÉE: (proudly) wazazi? Mimi ndio mzazi wake kwa hivyo hiyo barua niandikie mimi.

55. TEACHER: (confused) Uh? Unataka kuleta utani siyo?

56. DESIRÉE: (proudly) Siyo mwalimu huo ndio ukweli! Mama yetu alifariki yangu majuma manne yaliyopita. Mimi nina mikaka 16 na ndio mlezi wa ndugu yangu pamoja na nyanya yangu.

57. TEACHER: Nasikitika kuhusu kifo cha mama yenu. Lakini hakikisha kuwa mdogo wako analala mapema na pia lazima aoge kwani hata walimu wengine wanalalamika pia.
58. SFX: Footsteps leaving
59. DESIRÉE: (angry) Oh, mwalimu huyu kisirani kweli. Yeye anatoka mjini kwa hivyo hajui kabisa jinsi sisi tunavyoishi. Hana hata habari.
60. LORRAINE:(calm) Njoo rafiki yangu! Usiwe na huzuni. Yeye ni mwalimu na jukumu lake ni kumfanya Endurance atimize kazi zake za shule.Kwa hivyo ni sawa yey kusema. Angalia,– bado hatujaimba! beti moja tulikuwa wenyewe tunarap kabla hajaja kutukatiza! Ulikuwa unaimba sauti gani vile? (Singing)
61. CROSS FADE SINGING WITH CONVERSATION

Sc. 6 At home.

62. SFX: Evening ambience. Interior. FADE IN DIALOGUE
63. GRANMA: Lo ikiwa hivyo ndivyo walimu wanavyofikiria basi itakubidi uache shule, Desirée, ili upate kumshughulikia Endurance na watoto

wengine. Umeshasoma kwa miaka kumi sasa Mwache Endurance apate fungu lake nae na wewe ufanye kazi za shamba. Hata mimi nilifanya hivyo hivyo. Nilifika darasa la nane tu.

- 64. DESIRÉE:** Samahani nyanya, lakini nina hakika kuwa Mama alitaka tupate elimu ya kutosha. Alitaka mimi niendeleo na masomo pia. lakini... nitafikiria jinsi atutakavyo gawana kazi sawa kwa sawa.
- 65. GRANMA: (grumpy)** Eti sawa kwa sawa! Pah! Upuuzi huo wa usawa utakufikisha wapi? Lazima tuzingatie utamaduni wetu, Desirée. April alikuwa mama mwema. Ufuate mfano wake.
- 66. DESIRÉE:** nafahamu, Nyanya, lakini mama yangu alisema kuwa alijuta kukatiza masomo yake kwa ajili ya kuolewa huku akiwa na umri mdogo.
- 67. GRANMA:** Ndio, lakini yeye alitii alichambiwa. Tulimchagulia Babu kwa sababu alikuwa mkulima mwenye mafanikio. Ameporomoka katika wakati huu mgumu, lakini alikuwa mume mzuri. Alimtimizia kila kitu. Wala hakuwa na wasiwasi.

68. DESIRÉE: (with emphasis) Alikuwa na watoto sita lakini, watatu wakafariki dunia hayo ni majonzi makubwa.

69. GRANMA: ilikuwa ni kudra ya Mungu. Yeye ndie anaatupangia na wala hatupaswi kuhoji mipango hiyo.

70. DESIRÉE: (grumpy) Sisi tunafunzwa shuleni kuwa wadadisi.

71. GRANMA: Mungu anatuonyesha yale anayaotaka tuyajuwe mjukuu wangu.

72. **SFX:** SOFT EVOCATIVE MUSIC WITH CHOIR. FADE UNDER NEXT SCENE

NARRATOR: Desirée alipozongwa na hasira na upweke, alikuwa akienda kwenye bustani ambako kule alipata utulivu – chini ya miembe. Miti hiyo aliota mara kwa mara kwenye ndoto zake. Kila mti uliwakilisha wahenga katika familia yake na maisha jinsi yalivyo endelea kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Alihisi kana kwamba majani yaliyopeperushwa na upepo yalimnong’oneza masikioni mwake maneno haya – “Maisha yako ni yako”.

73. **SFX:** MUSIC UP (Des singing a soft song which is the signature tune: See attachment)

OUTRO.

Na mpaka hapo ndio tumefikia mwisho wa sehemu ya kwanza ya mchezo kwa jina “Chini ya Miembe” . Mchezo huu umetungwa na kuandikwa na Romie Singh. Usikose kujiunga na katika sehemu ya pili wakati amabapo Desirée anapata habari kuhusu mashindano murua katika Televisheni ya kutafuta vipaji katika jimbo lao.

Iwapo unataka kuusikiliza tena mchezo huu au labda ungependa kumjulisha rafiki yako ausikilize fungua tovuti yetu kupitia anuani ifuatayo dwworld.dedemkwaju.lbe. Hadi wakati mwingine, kwaheri.

END OF EPISODE ONE